**KISWAHILI**

Karatasi ya 2

**Machi, 2013**

Muda: Saa 2 ¼

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SHULE YA UPILI YA WASICHANA YA ALLIANCE**

**MTIHANI WA KABLA YA MWIGO**

**MACHI, 2013**

**Hati ya Kuhitimu Masomo ya Sekondari**

KISWAHILI

Karatasi ya 2

Ufahamu, Muhtasari, Lugha na Isimujamii

***MAAGIZO***

- Jibu maswali yote
- Karatasi hii ina sehemu nne
- Majibu yote yaandikwe kwenye nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali
- Karatasi hii ina kurasa 11

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| **SEHEMU** | **ALAMA** | **TUZO** |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

1. **UFAHAMU**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Mojawapo ya vipengee muhimu ambavyo mwalimu wa mwanafunzi wa Isimujamii anahitaji kujua ni historia ya Kiswahili. Katika kuangazia historia ya lugha hii muhimu ya Afrika Mashariki na kati mwalimu na mwanafunzi wake hawawezi kukwepa suala la jinsi Kiswahili kimeathiriwa na lugha nyingine.

Utafiti wa akiolojia au historia chimbo umeonyesha kwamba vyungu vya Wachina, maandishi ya Wamisiri na hata athari za wageni wengine kwa wakaazi wa pwani bado zingalipo. Aidha, historia imedokeza kwamba baadhi ya wageni hawa walipiga kambi na kuishi pwani ya Afrika Mashariki mapema mwaka 900 baada Kristo.

Wageni hao ambao walihamia pwani ya Afrika Mashariki kwa sababu wanazozijua wao wenyewe – waliishi katika eneo hilo na kufunga ndoa na wenyeji wa sehemu hizo. Wanavyosema Chiraghddin Shihabdin na Mathias Mnyapala katika historia ya Kiswahili, wahamiaji hao walichangia katika kupanuka na kukua kwa miji ya mwambao ya Waswahili kama vile Pate, Lamu, Mombasa, Kilwa, Vumba, Pemba na Zanzibar. Wajukuu wa Waarabu wengi pamoja na Waajemi *chambilecho* Abdala Khalid, walisahau lugha zao baada ya muda mrefu na kuanza kutumia Kiswahili. Hali ambapo lugha za baadhi ya wahamiaji hao "zilimezwa" na lugha ya wenyeji wa mwambao kimsingi ilitokana na uchache wao.

Hata hivyo Kiajemi au Washirazi kutoka Irani walipokeza Kiswahili maneno mengi mbayo yanapatika katika lugha hii hadi wa leo. Himaya ya Shirazi na makazi yao kuanzia kisiwa cha Funzi kusini mwa pwani ya Kenya hadi Tanga na Bagamoyo nchini Tanzania ingali inatambulika ingawa sio kwa njia *kinagaubaga* hivi leo.

Washirazi walitofautishwa na wakaazi wengine wenyeji wa pwani kama vile Wadigo na Wasegeju kwa sababu ya jinsi walivyoishi maisha yao kijumla. Walitengemea uvuvi na kutumia lahaja ya kipekee ya Kiswahili iliyojulikana kama Chichifundi.

Washirazi waliathiri Leksikoni ya Kiswahili katika mawanda mbalimbali. Mawanda na nyanya hizo ni pamoja na utawala ambapo tunapata maneno kama vile jumbe, diwani, waziri, serikali, shehe, akida, Amir na Sultan.

Katika mawanda ya biashara, Washirazi walichangia maneno kama vile tajiri na bakshishi. Kwenye mawanda ya uchukuzi kwa vyombo vya majini tunapata maneno kama vile bandari, nanga, tezi na kadhalika. Katika taaluma ya mimea, Washirazi walichangia maneno kama mbangi, mbilingani, mdengu, mgulabi, mharagwe, mpopo, mtambwi, mnazi,mdalasini na derabi. Kuhusu vyakula walichangia maneno kama birinzi, borohoa, gubiti, sambusa na siki. Msamiati wa mavazi, mapambo na rangi waliochangia ni pamoja na lasi, seredani, utaji, zari, zumari, urujuani na rangi.

Aidha, kwenye taaluma ya ujenzi walichangia maneno kama vile dari, boma, ghala na roshani. Maneno mengine ni bahati, usafidi, huruma, beluwa, hoihoi, ushenzi, barabara miongoni mwa mengine. Tathmini ya maneno haya inadhirisha kwamba asilimia tisini ni nomino.
Ni rahisi kwa lugha kukopa nomino kwa sababu kwamba Washirazi waliishi na kutangamana kwa urahisi na watu wengine Afrika ya Mashariki,

Waswahili walipokea vyema maneno ya lugha yao ambayo mengi yamekumbatiwa na kutumika sana hivi leo. Hii ni ishara kwamba *tamaduni* za watu hazina budi kuathiriana.

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

Maswali

a) Yape makala haya anwani mwafaka. (alama 2)

........................................................................................................................
........................................................................................................................

b) Toa ushahidi unaoonyesha kuwepo kwa wageni ambao waliathiri lugha ya Kiswahili katika mwambao wa Afrika Mashariki. (alama 2)

........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................

c) Ni kwa nini Waswahili walikubali na kukopa maneno mengi kutoka kwa Washirazi? (alama 2)

........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................

d) Lugha za kigeni ziliathiri lugha ya Kiswahili kwa njia chanya. Eleza. (alama 2)

........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................

e) Eleza mchango wa Washirazi kwa lugha ya Kiswahili. (alama 4)

........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................

f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa. (alama 3)

i) Chambilecho

........................................................................................................................

ii) Kinagaubaga

........................................................................................................................

iii) Utamaduni.

........................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

## 2. MUHTASARI (alama 15)

**Soma makala haya kisha ujibu maswali yanayofuata**

Kazi za fasihi simulizi, kama jina lilivyobainisha, zimejikita katika masimulizi ya mdomo. Hali kadhalika, kazi hizi huhifadhiwa bongoni au akilini. Uhifadhi wa namna hii una matatizo mengi. Hii ni kwa kuwa kumbukumbu za akilini zinaweza kufifia. Maisha tunayoishi siku hizi yana mambo mengi yanayoweza kuzifanya kumbukumbu za akilini kufifia. Kuna ajali za barabarani ambazo zimeathiri watu wengi kiakili, hivi kwamba wanapoteza fahamu zao. Hali kadhalika, maisha ya sasa yana mtifuko ambao unaathiri kumbukizi za watu. Mambo haya yakitokea kwa fanani ambaye anahifadhi hazina kubwa ya fasihi ni hasara kubwa.

Fauka ya hayo, vifo hutokea. Vinapotokea kwa mafanani wanaotegemewa katika kazi za fasihi simulizi, huwa hasara kubwa. Hii ni kwa sababu fasihi simulizi inaweza kupotea. Fauka ya haya, kuna tatizo la aliyehifadhi kazi kubadili umbo muhimu anaposimulia. Ubadilishaji huu unaweza kugeuza maana au kiini cha kazi hiyo ya fasihi simulizi. Hivyo, kazi itakosa ladha na faida kwa jamii. Licha ya hayo, namna kazi hiyo inavyozidi kusimuliwa kwa watu wengi ndivyo inavyopoteza asili yake. Matokeo ni hasara kubwa kwa vizazi vya baadaye.

Ili kuepuka matatizo kama haya, ni vizuri kuzihifadhi kazi za fasihi simulizi. Siku hizi kuna maendeleo ya teknolojia ambayo yanaweza kutoa msaada mkubwa katika kuzihifadhi kazi hizi kama vile mashairi, nyimbo, hadithi, methali, vitendawili na kadhalika. Zinaweza kuhifadhiwa kwenye kanda za sauti, video, filamu na hata sidii. Njia hizi zitahifadhi kazi hizo katika hali zao za asilia.

Tatizo ni kuwa njia hizi ni ghali, si wati wengi wanaweza kuimudu hali hii. Pia mitambo mingi inayotumia huhitaji utaalamu a ujuzi wa hali ya juu. Ni wanafunzi wangapi wa sekondari wana utaalamu kama huu?

Njia nyingine ya kuhifadhi kazi za fasihi simulizi ni kupitia kwenye maandishi. Hata hivyo, njia hii ina matatizo mengi. Kwanza, katika maandishi, sauti asilia ya masimulizi hupotea. Kwa hivyo inamhitaji msomaji kuongeza sauti na mahadhi yake mwenyewe. Hili nalo linaweza kuharibu au kufifilisha ubora wa kazi iwapo msomaji si mzuri katika kutia sauti au mahadhi. Hali hii huifanya kazi kupoteza uhalisia wake. Isitoshe, maandishi bora ni machache. Lakini utafanya nini iwapo mafundi wa fashi simulizi hawapo. Kuna wazee wengi sana vijijini wenye hazina kubwa ya kazi za fasihi simulizi. Ubaya ni kuwa hawafahamiki. Pana haja kufanya utafiti na kuwasaka wajuzi hawa ili watoe mchango wao katika uhifadhi wa kazi hizi.

Ukusanyaji hufanywa kwa utaratibu fulani. Kwanza, lazima kubainisha mtindo upi unafaa kutumia. Kuna mtindo kama utazamaji, matumizi ya hojaji, mahojiano na kushiriki. Katika utazamaji, mchunguzi anatakiwa kuwa na kalamu na karatasi. Hurekodi au kunasa yote yanayotendwa katika kazi fulani ya fashi simulizi.

Hojaji inapotumika, utayarishaji wake ufanywe mwanzo juu ya kile kinachotakiwa kuhifadhiwa kutegemea malengo ya utafiti. Hatimaye, mafanani wapewe hojaji hiyo. Mchunguzi anaweza pia kuwafanyia mafanani mahojiano na kuijaza. Kwa wale wasiojua kusoma na kuandika, mtafiti awaelekeze na kunakili mchango wao.

Mtindo wa nne unahitaji mkusanyaji kuwa mshiriki katika utendaji. Hivyo huhitajika kuwa mshiriki katika hadhira na wakati huo ashiriki katika utendaji. Lakini mtindo huu hukabiliwa na matatizo fulani. Kuna mambo katika jamii ambayo huzuia mchunguzi kushiriki katika utendaji wa kazi fulani ya fasihi simulizi. Mathalan katika sherehe ya jando, wasiotoka katika jamii hiyo na wale ambao hawajaipitia shughuli hiyo, hukatazwa kushiriki au kufanya utafuti. Wanaoshiriki nao

huapishwa wasichafua waliyoyaona au kukuyasikia. Ni vizuri mchunguzi kujua vizuizi kama hivi ajue namna atakavyokwepa.

Asili ya mikusanyo ya fasihi simulizi yaweza kuwa katika karamu na sherehe kama vile arusi, jando mazishi ,a kadhalika. Ni muhimu vijana wahudhurie sherehe kama hizi ili wajifunze mengi kuhusu fasihi simulizi.

(a) Fupisha aya tano za kwanza za makala haya (maneno 75 – 80) (alama9, utiririko1)

(b) Matayarisho

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

Jibu

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

(c) Ukirejelea aya mbili za mwisho, fafanua mambo muhimu ambayo mwandishi ametoa kuhusu ukusanyaji wa data ya fasihi simulizi. (Maneno 45 – 50) (alama 4, utiririko, 1)

Matayarisho

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

Jibu

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

3. **MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)**

(a) Tofautisha sauti zifuatazo: (alama 1)

(i) /v/.......................................................................................................................

(ii) /f/.......................................................................................................................

(b) Onyesha mtendwa, mzizi na viambishi tamati katika neno hili. (alama 3)

Limchialo

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

(c) Unda nomino nyingine kutokana na nomino: (alama 2)

(i) Mfadhili

.............................................................................................................................

(ii) Hatibu

.............................................................................................................................

(d) Onyesha kihusishi na utaje ni cha aina gani (alama 1 )

Sijamwona Faria tangu asubuhi

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

(e) Eleza muundo wa silabi zipatikanazo katika neno lifuatalo: (alama 3)

Biashara

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

(f) Tunga sentensi moja kubainisha maana mbili za neno **'sura'** (alama 2)

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

(g) Eleza tofauti kati ya sentensi hizi (alama 2)

(i)Miembe yote imekatwa

(ii)Miembe yoyote imekatwa

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................



For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

(h) Tambua nomino katika sentensi hii na utaje ni za aina gani (alama 2)

Isingekuwa ni kujitolea kwake, mazingira haya yangekuwa machafu.

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(i) Andika kinyume (alama 2)

Bwana Ali alimtaliki Zainab kabla ya fungate yao kuanza.

..............................................................................................................................

(j) Tambua kitenzi kilichopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo (alama 1)

<u>Huenda</u> tukala wali leo.

..............................................................................................................................

(k) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiunganishi **'japo'** (alama 1)

Wawili hao walipendana sana. Wawili hao hawakufunga ndoa

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(l) Tunga sentensi nne ukitumia **'–zuri '** kuonyesha matumizi yake kama: (alama 2)

Nomino..............................................................................................................

..............................................................................................................................

Kiwakilishi..........................................................................................................

..............................................................................................................................

Kivumishi............................................................................................................

..............................................................................................................................

Kielezi.................................................................................................................

..............................................................................................................................

(m)Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi (alama 3)

Vibanzi vitamu ajabu vimepikwa na mpishi.

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

(n) Sahihisha sentensi ifuatayo (alama 2)

Mbunge aliechaguliwa aliwapea fungu la leso wamama wote waliomfanyia kampeni.

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(o) Geuza sentensi ifuatavyo iwe katika usemi halisi (alama 2)

Rosa alisema kuwa yeye alikuwa mwanafunzi hodari na kuwa angefanya vyema katika mtihani waliokuwa wakisubiri.

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(p) Taja matumizi mawili ya mshazari (alama 1)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(q) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya hali isiyodhihirika (alama 1)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(r) Andika upya kulingana na maagizo (alama 2)

Paka ambaye alitipotiwa kupotea alipatikana kwenye bwawa la maji.

Anza: Katika bwawa...

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

(s) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa wingi (alama 2)

Ngoma inazopigwa imemshtua mtu.

....................................................................................................................................

(t) Kirai ni nini? (alama 1)

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

(u) Onyesha shamirisho kipozi na shamirisho kitondo katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Nyundo aliyotumia seremala kumjengea baba nyumba, imepotea.

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

(v) Kiambishi KI kimetumikaje katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Chakula kilichopikwa hakiliki.

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

**4. ISIMUJAMII (alama 10)**

(a) Taja na ueleze njia nne zinazochangia kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini (alama4)

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................



For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

(b) Eleza changamoto 3 zinazokumba Kiswahili katika ukuaji wake nchini (alama 3)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................

(c) Eleza maana ya istilahi zifuatazo (alama 3)

(i) Wingi – lugha

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(ii)Lahaja

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(iii)Ujozi-lugha

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com